**East African Journal of Swahili Studies**
eajss.eanso.org
**Volume 8, Issue 2, 2025**
**Print ISSN: 2707-3467 | Online ISSN: 2707-3475**
Title DOI: https://doi.org/10.37284/2707-3475

EAST AFRICAN NATURE & SCIENCE ORGANIZATION

*Original Article*

# Unyanyasikaji wa Wanaume katika Diwani za Tumbo Lisiloshiba na Maskini Milionea na Hadithi Nyingine

*Elizabeth Wanjiru Waithaka[1*], Dkt. John Khaisie Wanyama, PhD[1] na Dkt. Timothy Kinoti M'ngaruthi, PhD[1]*

[1] Chuo Kikuu cha Embu, S. L. P. 6-60100, Embu, Kenya.
[*] ORCID ID; https://orcid.org/0009-0005-7045-8281; Barua pepe ya mawasiliano: ewwanjiru84@gmail.com

**DOI ya Nakala: https://doi.org/10.37284/jammk.8.2.3257**

**Tarehe ya Uchapishaji:**

*03 Julai 2025*

**Istilahi Muhimu**:

*Unyanyasikaji, Wanaume, Mtagusano wa Vitambulisho, Uchumi, Jinsia.*

**IKISIRI**

Fasihi kama kioo cha jamii hutumia lugha kwa ufanifu mkubwa kutuchorea taswira kamili ya yale yanayotendeka katika jamii. Fasihi haizuki katika ombwe tupu. Hivyo basi utafiti huu ulichunguza unyanyasikaji wa wanaume katika jamii. Ulichunguza suala mtambuko ambalo linaathiri haki za wanaume kama inavyosawiriwa katika Diwani ya Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine iliyohaririwa na Alifa Chokocho na Dumu Kayanda na Maskini Milionea na Hadithi Nyingine iliyohaririwa na Ken Walibora. Lengo kuu la makala hii ni kuchunguza namna wanaume hunyanyasika katika diwani teule. Ilikuafikia lengo hili, nadharia ya Mtagusano wa Vitambulisho ilitumiwa. Ni mojawapo ya nadharia za kijinsia. Utafiti huu ulikuwa wa kimaktaba. Data ya utafiti ilikusanywa kwa kusoma hadithi teule kutoka diwani za Kiswahili zilizoteuliwa vitabu, majarida na makala mengine kutoka mitandaoni. Uteuzi wa sampuli ulikuwa wa kimaksudi. Data iliyokusanywa ilichanganuliwa kimaelezo kwa kutumia mbinu ya uchanganuzi matini ikiongozwa na madhumuni ya utafiti. Matokeo ya utafiti yaliwasilishwa kwa njia ya kimaelezo. Matokeo ya makala yalionyesha kuwa mwanamume hunyanyasika kwa namna nyingi kama vile: kula uroda nje ya ndoa, utengano wa kijamaa, kukataliwa uchumba, upyaro, kunyimwa chakula na kuchapwa. Vipengele vya utambulisho vinavyoshirikiana na kusababisha unyanyasikaji wa wanaume ni: uchumi, jinsia, tabaka, matarajio ya kijamii. Kipengele kinachosababisha unyanyasikaji wa wanaume zaidi ni kipengele cha uchumi. Uchunguzi huu utawafaa wasomi, wanajamii, na waandishi kwani watapata uelewa zaidi wa aina za unyanyasikaji unaotendewa wanaume na kutafuta mbinu za kuwaokoa kutoka kwa udhalimu huu. Vile vile utakuwa na mchango katika taaluma ya fasihi ya Kiswahili.

**APA CITATION**

Waithaka, E. W., Wanyama, J. K. & M'ngaruthi, T. K. (2025). Unyanyasikaji wa Wanaume katika Diwani za Tumbo Lisiloshiba na Maskini Milionea na Hadithi Nyingine. *East African Journal of Swahili Studies*, *8*(2), 37-52. https://doi.org/10.37284/jammk.8.2.3257

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.8.2.3257

**CHICAGO CITATION**

Waithaka, Elizabeth Wanjiru, John Khaisie Wanyama and Timothy Kinoti M'ngaruthi. 2025. "Unyanyasikaji wa Wanaume katika Diwani za Tumbo Lisiloshiba na Maskini Milionea na Hadithi Nyingine". *East African Journal of Swahili Studies* 8 (2), 37-52. https://doi.org/10.37284/jammk.8.2.3257

**HARVARD CITATION**

Waithaka, E. W., Wanyama, J. K. & M'ngaruthi, T. K. (2025) "Unyanyasikaji wa Wanaume katika Diwani za Tumbo Lisiloshiba na Maskini Milionea na Hadithi Nyingine", *East African Journal of Swahili Studies*, 8(2), pp. 37-52. doi: 10.37284/jammk.8.2.3257

**IEEE CITATION**

E. W., Waithaka, J. K., Wanyama & T. K., M'ngaruthi "Unyanyasikaji wa Wanaume katika Diwani za Tumbo Lisiloshiba na Maskini Milionea na Hadithi Nyingine", *EAJSS*, vol. 8, no. 2, pp. 37-52, Jul. 2025.

**MLA CITATION**

Waithaka, Elizabeth Wanjiru, John Khaisie Wanyama & Timothy Kinoti M'ngaruthi. "Unyanyasikaji wa Wanaume katika Diwani za Tumbo Lisiloshiba na Maskini Milionea na Hadithi Nyingine". *East African Journal of Swahili Studies*, Vol. 8, no. 2, Jul. 2025, pp. 37-52, doi:10.37284/jammk.8.2.3257.

## UTANGULIZI

Unyanyasaji hasa katika familia ni ukatili unaotokea mara kwa mara na watu wote hunyanyasika wakiwemo wanawake, wanaume na watoto. Unyanyasaji ni kinyume chahaki na usawa. Ni kumfanyia mtu vitendo vya dharau na dhuluma kwa kumnyima haki zake. Unyanyasikaji katika jamii ni jambo ambalo limekuwa likiendelea kwa muda mrefu.

Kwa mujibu wa utafiti huu, unyanyasikaji dhidi ya wanaume ni hali ya wanaume kuteseka kwa sababu ya kutendewa vitendo vya kuwadhalilisha au kwa sababu ya hali yao kama wanaume. Hili ni suala mtambuko katika jamii na linafaa kuchunguzwa kwani ni uhalisia wa mambo ingawa idadi kubwa ya wanaonyanyaswa wanalinyamazia jambo hili. Matei (2017) anasema kuwa mwanamume ananyanyasika katika jamii na nafasi yake haitambuliki.

Ortiz (2021) alieleza kwamba wanaume wanaweza kukandamizwa kwa sababu ya kuwa wanaume. Anatoa madai kuwa yale ambayo wanaume hupitia hayaangaziwi. Anasema swali lolote kuhusu ukandamizaji wa wanaume lazima liangaziwe kwa kuwa wanaume huathirika pia wanapopitia matatizo. Anaeleza kuwa ukandamizaji wa wanaume ni mfano wa wanaume kukandamizwa kama wanaume.

Taylor (2023) alisema kuwa mauaji ya msanii AKA ni kengele ya kuiamsha Afrika Kusini. Anasema kuwa uhalifu na unyanyasaji nchini Afrika Kusini hutofautiana kulingana na jinsia ya mwathiriwa. Wanaume na wanawake hupitia hali hii kwa njia tofauti. Anaeleza kuwa ingawa wanaume wana uwezo mkubwa wa kuua wakati wa vurugu, wako katika hatari kubwa ya kuuawa nyumbani mwao na wapenzi wao wa karibu. Vilevile wako katika hatari ya unyanyasaji wa kijinsia. Alisema bila kujali kuwa na wakati wa vurugu, kila wakati mhalifu ni mwanamume. Alieleza mwanamume hulaumiwa kila wakati kunapozuka jambo baya.

Bahemu (2021) anasema ukizungumzia unyanyasaji wa kijinsia wengi huwaza kwa upande mmoja, kwamba ni dhidi ya mwanamke lakini uhalisia ni tofauti kwani hata wanaume hunyanyaswa isipokuwa si wepesi kuzungumza. Haya yalielezwa wakati wa kongamano la kupinga ukatili wa kijinsia lililoandaliwa na *Norwegian Church Aid* (NCA) mkoani Manyara. Ilikuwa sehemu ya maadhimisho ya siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsia. Katika kongamano hilo lililohudhuriwa na viongozi wa dini, wanaharakati, wazee na viongozi wa serikali, mwakilishi wa kamanda wa polisi alisema kuwa wanaume hunyanyaswa isipokuwa hawasemi.

King'ei (2002) anasema kuwa suala la udhalilishaji wa wanawake limepewa uzito wa kutosha katika

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.8.2.3257

utafiti wa Kiswahili hadi sasa, kwa hivyo kuna haja ya kuangazia upande wa pili wa sarafu kwa kuzingatia namna waandishi wa kike wanavyoumba wahusika wa kiume. Jambo hili ni muhimu kwa vile wasomi wengi katika uwanja huu wameshikilia kuwa ubaguzi wa kiuana ni wa upande mmoja tu, madai ambayo si ya kweli.

Licha ya kuwepo unyanyasikaji wa jinsia zote, udurusu uliofanywa wa tafiti za awali kuhusu masuala ya uana ulidhihirisha kuwa kuna tafiti chache zilizofanywa kuhusiana na unyanyasikaji dhidi ya wanaume. Watafiti na waandishi wa masuala ya uana wameangazia mada zinazowahusu wanawake na watoto. Ni vyema kutambua kuwa unyanyasikaji wa wanaume ni uhalisia wa mambo katika jamii. Matei (2017) anasema kuwa nafasi ya mwanamume haitambuliki katika jamii. Makala hii inajadili unyanyasikaji wa wanaume kama unavyoakisiwa katika diwani za Tumbo lisiloshiba na Maskini Milionea.

**MAPITIO YA MAANDISHI**

Parhiala (2021) Mkurugenzi wa NCA alieleza unyanyasaji kama uvunjifu wa haki za binadamu, uhalifu, makosa ya kimaadili na hakuna faida yoyote zaidi ya madhara ya muda mfupi na muda mrefu. Kwa mtu binafsi, unyanyasaji husababisha mshtuko wa kihisia, majeraha ya kimwili, magonjwa ya zinaa, ulemavu, matatizo ya afya, mimba zisizotarajiwa na hata kifo.

Alberta (2021) anasema katika ndoa kuna unyanyasikaji ambapo mpenzi mmoja hutawala, kuonea au kudhalilisha mwingine. Unyanyasikaji wa kihisia ni kuvunja mtu moyo, kudhibiti fedha kumtenga mpenzi wake na kuzuia uhuru wake. Unyanyasaji wa kimwili ni pamoja na shughuli yoyote ambayo inaweza kuleta maumivu ya kimwili au kujeruhiwa. Unyanyasaji wa kijinsia ni pamoja na kutumia nguvu ili kupata mpenzi kwa njia zisizo za haki, kukejeli au kukosoa utendaji wake na kumnyima mapenzi. Kutumia vitisho pia ni aina ya unyanyasaji ambapo mpenzi hutumia maneno au matendo kumtishia mwenzake kama vile: kuharibu mali na kumweka mtu wasiwasi.

Laititi (2005) amefanya utafiti juu ya unyanyasaji wa wanaume ambao wamestaafishwa mapema. Ana maoni kuwa visa vya wanawake kuwanyanyasa wanaume wao vimeongezeka kwa sasa. Amebainisha kuwa baadhi ya wanaume waliofutwa kazi hutumikishwa na wake zao ambao wanachukulia kuwa mwanamume kukosa uwezo wa kiuchumi ni sawa na kushushwa hadhi kama kiongozi wa nyumba. Baadhi ya wanawake hawa huwaachia wanaume zao kazi za nyumbani na wengine hukataa kufuatana nao katika kumbi za starehe na badala yake huandamana na wanaume wengine walio na hadhi ya juu kama wao. Anasema kuwa mwanamume ambaye tayari nafsi yake imehasiriwa na hali yake mpya kama kustaafu halafu wanaachwa nyumbani bibi zao wanapoenda katika kumbi za starehe ni kumtesa kwa kiwango kikubwa.

Gitau (2005) alitafiti kuhusu unyanyasaji dhidi ya wanaume katika fasihi ya Kiswahili. Alisema wanaume hukabiliwa na unyanyasaji wa kutukanwa na wake zao, wake wengine au wanaume wengine. Matusi haya hutokana mara nyingi na yale majukumu mwanaume aliyopewa na jamii kama mkimu familia yake. Alisema pia wanaume hukabiliwa na unyanyasaji wa kutengwa na familia walimokulia na watu wengine wanaohusiana nao kidamu.

Ruto (2015) amefanya utafiti juu ya matatizo ya mwanamke katika riwaya ya *Kidagaa Kimemwozea na Nguzo za Mama*. Anasema jamii nyingi za Kiafrika huchukulia mwanamke kama kitega uchumi. Kabla ya kuolewa ni lazima mahari ilipwe kama dhamana na hili husababisha wasichana kuozwa mapema. Alisema pia wanawake hunyanyaswa kwa kudharauliwa. Mwanamke ana haki ya kuheshimiwa na kudhaminiwa kwani anachangia katika maendeleo na kuchuma mali katika jamii. Dharau inajitokeza pale ambapo mke anakosa kuthaminiwa, kuvunjiwa heshima na

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.8.2.3257

kuaibishwa kupitia vitendo anavyotendewa na lugha anayoelekezewa. Wanawake pia hunyanyaswa kimapenzi. Utafiti wake ulipendekeza kuwa utafiti wa baadaye uchunguze iwapo wanaume hunyanyaswa katika fasihi andishi.

**NADHARIA YA UTAFITI**

Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Mtagusano wa Vitambulisho. Ni mojawapo ya nadharia za kijinsia. Nadharia ya kijinsia haihusu tu kutetea haki za wanawake. Inaweza kufaa kwa kuchanganua unyanyasikaji wa wanaume hasa wakati uchanganuzi unahusu matarajio ya kijinsia na mifumo ya mamlaka. Nadharia hii ni mfumo unaochunguza jinsi mamlaka, majukumu ya kijinsia na miundo ya kijamii inavyounda uzoefu kwa jinsia zote. Mitazamo mingi ya kijinsia kama vile Mtagusano wa Vitambulisho na ufeministi wa baada ya muundo hukagua jinsi mfumo dume hudhuru kila mtu wakiwemo wanaume.

Nadharia ya Mtagusano wa Vitambulisho iliasisiwa na Kimberlé Crenshaw ambaye ni mwanasheria na msomi wa masuala ya haki za kiraia. Aliitambulisha rasmi mnamo 1989 katika makala yake yenye kichwa *Demarginalizing the Intersection of Race and Sex*, ambapo alieleza jinsi wanawake weusi walivyokumbwa na aina tofauti za ubaguzi ambazo haziwezi kueleweka kwa kutumia mtazamo mmoja tu wa jinsia au rangi.

Crenshaw alianzisha nadharia hii ili kueleza jinsi mifumo ya ukandamizaji inavyoshirikiana na kuathiri watu kwa njia nyingi. Aliona kwamba sheria na harakati za kijamii zilikuwa zinashughulikia ubaguzi wa rangi na ubaguzi wa kijinsia kama mambo tofauti, bila kuzingatia jinsi mtu anavyoweza kukumbwa na aina zote mbili za ubaguzi kwa wakati mmoja. Alitoa mfano kuwa, wanawake weusi walikuwa wakikumbwa na changamoto ambazo zilikuwa tofauti na zile zinazowakumba wanawake wa rangi nyingine au wanaume weusi. Hivyo, Crenshaw alisisitiza kwamba ukandamizaji hauwezi kuchambuliwa kwa kutenganisha vipengele vya utambulisho wa mtu, bali kwa kuzingatia jinsi vinavyoshirikiana na kuathiriana. Nadharia hii hutumika katika jamii za kisasa kwa njia mbalimbali, hasa katika masuala ya haki za kijamii, sera za umma, na harakati za kijamii.

Patricia Hill Collins (1990) alichangia nadharia ya Mtagusano wa Vitambulisho kupitia kazi yake ya *Black Feminist Thought*. Katika kazi hii, alianzisha dhana ya matriki ya utawala ambayo inaeleza jinsi vipengele vya utambulisho kama jinsia, rangi, na tabaka vinavyoathiriana na kuunda mifumo ya ukandamizaji. Collins alipanua nadharia ya mtagusano wa vitambulisho kwa kuonyesha jinsi wanawake weusi wanavyokabili ukandamizaji wa kimfumo kwa njia tofauti na wanawake wa jamii nyingine, akisisitiza umuhimu wa kuzingatia mwingiliano wa vipengele vya utambulisho katika uchambuzi wa kijamii.

Audre (1984) alichangia nadharia ya Mtagusano wa Vitambulisho hasa kupitia maandiko yake ya kifeministi na kijamii, ingawa hakutumia neno mtagusano moja kwa moja. Yeye alizungumza kwa kina kuhusu maingiliano ya vitambulisho tofauti vya kijamii kama vile: jinsia, rangi, tabaka na mapenzi na jinsi vinavyoathiri uzoefu wa ukandamizaji au ukosefu wa haki. Kazi yake muhimu, *Sister Outsider: Essays and Speeches* (1984), ilichangia sana katika kuelewa jinsi vipengele vya utambulisho kama vile jinsia na rangi vinavyoathiriana na kuunda uzoefu wa ukandamizaji.

Katika maandiko yake, Lorde alisisitiza kuwa ukandamizaji hauwezi kuchunguzwa kwa mtazamo mmoja tu, bali unapaswa kuzingatia mwingiliano wa vipengele vyote vya utambulisho wa mtu. Kauli yake maarufu, *"The master's tools will never dismantle the master's house,"* ilihimiza harakati za kijamii kutambua na kushughulikia mifumo ya ukandamizaji kwa mtazamo mpana.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.8.2.3257

Nadharia ya Mtagusano wa Vitambulisho ina mihimili kadhaa inayosaidia kuelewa jinsi vipengele mbalimbali vya utambulisho wa mtu vinavyoshirikiana na kuathiri uzoefu wake wa kijamii. Mihimili hii ni msingi wa uchambuzi wa ukandamizaji na upendeleo katika jamii.

1. Mwingiliano wa vipengele vya utambulisho: nadharia ya Mtagusano wa Vitambulisho inasisitiza kwamba mtu anaweza kuwa na utambulisho zaidi ya mmoja, kama vile jinsia, rangi, hadhi, mwelekeo wa kijinsia, na ulemavu. Vipengele hivi vinavyoshirikiana vinaweza kuathiri jinsi mtu anavyopokea upendeleo au ukandamizaji katika jamii.

2. Ukandamizaji wa Kimuundo. Nadharia hii inaeleza jinsi mifumo ya kijamii, kisiasa, na kiuchumi inavyoweza kuendeleza ukandamizaji kwa watu wenye utambulisho tofauti. Mfumo wa sheria, elimu, na ajira unaweza kuwa na upendeleo unaoathiri makundi fulani kwa njia tofauti.

3. Uzoefu wa Kipekee wa Ukandamizaji. Nadharia ya Mtagusano wa Vitambulisho inaonyesha kuwa watu wenye utambulisho tofauti wanakumbwa na changamoto za kipekee ambazo haziwezi kueleweka kwa kutumia mtazamo mmoja tu wa ukandamizaji. Kwa mfano, mwanamke mweusi anaweza kukumbwa na changamoto ambazo ni tofauti na zile zinazowakumba wanawake wa rangi nyingine au wanaume weusi.

4. Uwakilishi na Sauti ya Makundi ya Kijamii. Nadharia hii inasisitiza umuhimu wa kuwapa nafasi watu kutoka makundi yaliyotengwa ili waweze kueleza uzoefu wao wenyewe. Uwakilishi katika vyombo vya habari, siasa, na elimu unapaswa kuzingatia mwingiliano wa vipengele vya utambulisho.

5. Mabadiliko ya Kijamii na Haki. Mtagusano wa Vitambulisho inahimiza mabadiliko ya kijamii kwa kuhakikisha kwamba sera na sheria zinazingatia mahitaji ya watu wenye utambulisho tofauti. Harakati za kijamii zinapaswa kujumuisha mtazamo wa Mtagusano wa Vitambulisho ili kuhakikisha kwamba zinawakilisha makundi yote kwa usawa.

## MBINU ZA UTAFITI

Utafiti huu ulitumia muundo wa kimaelezo. Utafiti ulikuwa wa kimaktaba. Mtafiti alikusanya data kwa kusoma kwa kina maandishi yanayohusu mada na pia kazi zilizoshughulikia mada hii. Alisoma kwa undani yaliyoandikwa kuhusu unyanyasikaji wa wanaume katika hadithi fupi teule za Kiswahili katika *Diwani ya Tumbo lisiloshiba*. na *Maskini Milionea* akiongozwa na nadharia ya Mtagusano wa Vitambulisho Usomaji wa tasnifu, majarida, magazeti, vitabu na kwenye mitandao ulifanywa ili kupata data faafu. Uteuzi wa sampuli ulikuwa wa kimaksudi. Sampuli iliyochaguliwa ni hadithi zilizoangazia suala la unyanyasikaji wa wanaume. Mtafiti alichanganua data kwa kutumia mbinu ya uchanganuzi matini. Data iliwasilishwa kwa njia ya maelezo.

## MATOKEO YA UTAFITI

Sehemu hii inaonyesha matokeo ya utafiti yaliyowasilishwa kwa kwa njia ya maelezo. Yalionyesha njia kadhaa ambazo kwazo wanaume hunyanyasika. Njia zilizobainika ni zifuatazo:

### Kula Uroda Nje ya Ndoa

Unyanyasikaji wa kwanza unaopitiwa na wanaume ni wake zao kutokuwa waaminifu na kushiriki uroda nje ya ndoa. Kula uroda nje ya ndoa ina maana ya kushiriki mapenzi nje ya ndoa. Uaminifu ni mojawapo ya misingi muhimu sana katika maisha ya binadamu hasa katika mahusiano ya kijamii, kibiashara na kikazi. Ni msingi wa kuaminika, kutegemewa, na kujenga uhusiano wa kudumu na wenye manufaa.

Lenard (2025) anasema kuwa uaminifu katika ndoa huwa na faida. Vilevile anasema uaminifu unapokosekana huleta mikinzano. Kulingana naye, faida za uaminifu ni kama vile: kujenga mahusiano imara, kuleta utulivu wa akili na furaha, kuaminika

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.8.2.3257

na kutegemewa na watu wengine, kupunguza migogoro na mivutano na kuweka mazingira bora ya kufanya kazi. Uaminifu ni nguzo ya mahusiano yenye afya na thabiti, iwe ni katika familia, urafiki au mahusiano ya kimapenzi

Mwandishi wa hadithi ya *Haramu tamu* katika diwani ya *Maskini Milionea*, amedhihirisha kuwa mwanamume ananyanyasika pale ambapo anapoendewa kinyume na mkewe.

Kama alivyobashiri, alijibu na wakakubaliana kukutana katika mkahawa alioupendekeza Chaurembo mwenyewe viungani mwa mji. Alitambua kuwa alikuwa mke wa mtu, ndio sababu akataka wakutane katika mkahawa wa faragha, mbali na upeo wa macho ya wateja wengine (MM, uk. 84)

Sentensi *Alitambua yeye ni mke wa mtu, ndio sababu akataka wakutane katika mkahawa wenye sehemu za faragha mbali na upeo wa macho ya wateja wengine* inadhihirisha kuwa Chaurembo alishiriki mapenzi nje ya ndoa. Chaurembo hakutaka kuonekana na mwanamume asiyekuwa mumewe. Wengi walifahamu kuwa alikuwa mke wa mtu. Hili linasababisha kupendekeza kuwa wakutane katika hoteli ambapo hakuna yeyote angemfahamu. Iwapo Chaurembo hakuwa na lolote alilotaka kulificha, hangeogopa kukaa katika hoteli ambapo watu wangemwona. Hangeogopa kuonekana na mpenzi wake wa kando. Ni wazi kuwa alikuwa akishiriki uroda nje ya ndoa.

Mwandishi anaonyesha Karisa akinyanyasika kwa kukosa usingizi na amani kwa sababu ya mkewe kurejea usiku. Anasema:

Moyo ulimpapa Chaurembo alipojipenyeza nyumbani mwake jioni hiyo. Kulikuwa na kimya kikuu. Isipokuwa taa za nje, ndani mlikuwa giza. Chaurembo akaamini Karisa mumewe alikuwa usingizini. “Umechelewa, mpenzi. Itakubidi upunguze kazi. Huu mji siku hizi usiku una wenyewe”. (MM, uk. 86)

Sentensi *Umechelewa, mpenzi. Itakubidi upunguze kazi.* inaashiria kuwa Karisa alikuwa ananyanyasika. Mkewe Chaurembo alikuwa akirejea nyumbani usiku wa manane. Karisa alinyanyasika kwa kuwa mwanamume. Unyanyasikaji ulitokana na yeye kutambua kuwa mkewe alikuwa akishiriki mapenzi ya nje ya ndoa.

Karisa hakuwa anapatwa na usingizi akimsubiri mkewe. Alinyanyasika pia kwa kukosa amani na utulivu. Alimweleza mkewe kuwa *Huu mji siku hizi usiku una wenyewe* kumaanisha kuwa kulikuwa na wezi usiku na ilikuwa hatari yeye kutembea usiku. Alihofia kuwa jambo mbaya lingemtendekea mkewe. Akamwonya dhidi ya kutembea usiku. Hili linaonyesha kuwa Karisa hana amani na ananyanyasika.

Crenshaw (1989) alieleza jinsi mifumo ya ukandamizaji inavyoshirikiana na kuathiri watu kwa njia nyingi. Alisema kuwa ukandamizaji hauwezi kuchambuliwa kwa kutenganisha vipengele vya utambulisho wa mtu, bali kwa kuzingatia jinsi vinavyoshirikiana na kuathiriana. Kulingana na nadharia, kipengele cha uchumi na jinsia vinashirikiana katika unyanyasikaji wa Karisa. Karisa anampa mkewe uhuru wa kufanya kazi ili kuchangia katika uchumi. Mkewe Chaurembo anaitumia nafasi hii vibaya na kuwa na mapenzi nje ya ndoa. Anaanza kurejea nyumbani akiwa amechelewa sana. Akiulizwa na mumewe amechelewa wapi anasema kuwa mikutano kazini imekuwa mingi. Anamdanganya mumewe kuwa alikuwa mikutano ya kikazi.Alikuwa akikutana na mpenzi wake wa kando wakichupa kutoka hoteli moja hadi nyingine. Mumewe Karisa ananyanyasika kwa kukosa usingizi mkewe anapochelewa. Hana amani pia. Anasubiri mkewe arudi akiwa amezima taa za nyumbani. Mkewe anadhani kuwa mumewe kesha lala.

Katika hadithi ya *Masharti ya Kisasa* katika *Diwani ya Tumbo Lisiloshiba*, tunamwona Dadi akinyanyasika sana kwa kudhani kuwa mkewe ana mpango wa kando. Mwandishi anasema:

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.8.2.3257

Lazima niache kazi maana mume wangu haniamini… Anadhani kwamba mimi nakwenda na… ananifikiria nina "mpango wa kando'' (TL, uk. 68*)*

Tunamwona Kidawa akienda kufuta kazi ya umetroni. Mumewe Dadi alidhani kuwa ana mpango wa kando ingawa Kidawa hakuwa nao. Mumewe Dadi anakuwa na wasiwasi mwingi kuwa mke wake ana jicho la nje. Anaamua kumfuata ilikwenda kuchunguza. Anamfuata Kidawa mpaka kazini. Aliamua kupanda paipu iliyotoka chini mpaka juu karibu na dirisha la mwalimu mkuu. Alijiambia lazima apande paipu ili achungulie vituko vinavyoendelea baina ya mkewe na mwalimu mkuu.

Mwandishi anaonyesha Dadi akinyanyasika kwa kupata majeraha anapomfuata mkewe kazini kuthibitisha iwapo ana mapenzi nje ya ndoa.

Alikuwa kalala chini kwenye kokoto na kupoteza fahamu. Kidawa alipopiga tochi alimkuta mumewe Dadi damu imemwenea kichwani. Mwalimu mkuu hakusita hapo kamwe. Haraka alikwenda kupiga simu kuita ambulensi. (TL, uk. 68)

Maneno *alikuwa kalala chini kwenye kokoto na kupoteza fahamu* na *damu imemwenea kichwani* yanaonyesha jinsi Dadi alinyanyasika kwa kumshuku mkewe kuwa na mpenzi wa kando. Dadi alishindwa kutulia. Akasema wanakijiji wanamsema kuwa amedhibitiwa na mke. Haya yalimkera Dadi sana mpaka akaamua kumfuata mkewe. Baadaye anaumia sana na kupelekwa hospitali. Hakuna jambo linaloweza kumkera mwanamume zaidi kama kujua kuwa mkewe ana mapenzi nje ya ndoa. Jambo hili husababisha hata wapenzi kuuana wanapogundua kuwa wanaendewa kinyume, jambo ambalo halifai. Dadi anachora taswira ya kiwango cha athari ambayo mwanamume hupitia akigundua kuwa mkewe ana mpango wa kando.

Kulingana na Crenshaw (1989) mifumo ya ukandamizaji hushirikiana na kuathiri watu kwa njia nyingi. Alisema kuwa ukandamizaji hauwezi kuchambuliwa kwa kutenganisha vipengele vya utambulisho wa mtu, bali kwa kuzingatia jinsi vinavyoshirikiana na kuathiriana. Kulingana na nadharia, Dadi ananyanyasika kwa sababu ya kipengele cha uchumi na jinsia. Mkewe Kidawa anapoenda kazi ya umetroni usiku, Dadi anashuku kuwa ana mpenzi wa kando. Ananyanyasika kwa sababu ya kuwa mwanamume. Unyanyasikaji huu unatokea Dadi anaposhuku kuwa mkewe ana mpango wa nje. Anapatwa na wivu na kuanza kumpeleleza. Baadaye anaumia sana na kupelekwa hospitali.

Msimamo wa mtafiti ni kuwa wanawake wanapopata nafasi ya kuchangia uchumi, wanafaa kuwa waaminifu kwa wapenzi wao. Si kutenda kama Chaurembo alivyofanya. Kupewa uhuru wa kufanya kazi naye akamwendea mumewe kinyume. Vilevile wanaume hawafai kuwashuku wake zao kuwa na mipango ya kando wanapoenda kazini Tunaona vile Dadi alinyanyasika kwa kumshuku mkewe. Aliishia hospitali na majeraha mabaya sana. Wakulaumiwa hapa ni wote wake kwa waume. Wanawake wanawaendea kinyume waume zao nao wanaume wanawashuku wake zao kuwa na mapenzi nje ya ndoa. Wanandoa wanafaa kuelimishwa umuhimu wa kuwa waaminifu katika ndoa. Vilevile kuhusu madhara ya kuwashuku wengine na kutokuwa waaminifu katika ndoa.

Katika hadithi ya *Mapenzi ya kifaurongo* katika diwani ya *Tumbo Lisiloshiba*, mwandishi anasema:

Wewe unasema kuwa kwetu kuna mali, hiyo ni kweli. Lakini nimekuwa na mpenzi ambaye kwao wana mali pia. Hata hivyo, baina yetu masikilizano yamekosekana, Hakuwa mwanimifu. Kutokana na hilo mimi nikaona nimwondokee. (TL, uk. 20)

Sentensi *Hakuwa mwanimifu. Kutokana na hilo mimi nikaona nimwondokee*.inaonyesha kuwa mpenzi wa Penina hakuwa mwaminifu. Penina anakuja kwa Dennis kumwomba awe mpenzi wake. Anamwambia kuwa moyo wake umedodokea

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.8.2.3257

kwake. Angependa awe rafiki yake wa chanda na pete, mpenzi wake wa dhati wa kumfaa na yeye kumfaa kwa jua na makali. Anamweleza kuwa alikuwa na mpenzi lakini akamwondokea. Dennis anashawishika na kukubali kuwa mpenzi wa Penina. Dennis anampeleka kuwaona wazazi wake nyumbani. Baadaye Dennis anapotafuta riziki na kukosa, tunamwona Penina akikosa kuwa mwaminifu kwake. Mwandishi anasema:

“Usiniite mpenzi. Tena tafadhali usije ukamwambia mtu uliwahi kuwa mpenzi wangu. Tafuta mwingine mwenye hali kama yako. Kwaheri mkata, kwaheri ya kuonana. Mungu atakupa mpenzi mwingine, aupakate ufukara wako, akuliwaze ufukara uliouzoea.

“Penzi letu je? Limekwenda wapi?” Nauliza

“Penzi lenu na nani?” Penina anajibu. “Mgomba changaraweni haupandwi ukamea. Potelea mbali mkata wee!” Penina anafoka kwa kiburi na dharau. ( TL, uk. 26)

Sentensi *Penzi letu je? Limekwenda wapi?” Nauliza “Penzi lenu na nani?” Penina anajibu* zinaashiria kuwa Dennis alikuwa akinyanyasika kwa sababu ya mpenziwe kutokuwa mwaminifu. Penina anapomfukuza nyumbani na kumwambia kuwa asiwahi kumwambia yeyote kuwa amekuwa mpenziwe, Dennis ananyanyasika na kumwuliza penzi lao lilienda wapi. Penina alimwendea Dennis awe mchumba wake. Mwanzoni Dennis anakataa wito huu na kumwambia Penina kuwa haiwezekani kwa sababu ya hali zao zisizofanana hata kidogo. Penina alitoka katika familia yenye nafasi. Naye Dennis kwao wanapigania mikono ielekee vinywani. Anamwambia kuwa mzoea vya sahani, vya kigae haviwezi. Hatimaye Dennis anakubali kuwa mpenzi wa Penina na wanaanza kuishi pamoja. Dennis anatafuta ajira kwa siku nyingi lakini hafanikiwi. Penina anaanza kubadilika na kuanza kutompa chakula. Baadaye Penina anamfukuza Dennis na kumwambia nyumba yao aione paa. Penina anakosa kuwa mwaminifu kwa Dennis licha ya kuwa yeye ndiye aliyeenda kumtafuta awe mpenzi wake. Hili ni dhihirisho kuwa wanaume wananyanyasika wake zao wanapokosa kuwa waminifu katika ndoa.

Mifumo ya ukandamizwaji huathiri waja katika jamii kulingana na Crenshaw (1989). Kipengele cha utambulisho cha tabaka na uchumi vinachangia kunyanyasika kwa Dennis. Mpenziwe Penina anamwendea na kumwomba awe mpenzi wake. Mwanzoni anakataa kwa sababu ya hali zao za kitabaka. Dennis ametoka tabaka la chini naye Penina ametoka tabala la juu. Wanaishi pamoja kwa furaha lakini baadaye Dennis anapokosa kazi kabisa mpenziwe anamfukuza na kumweleza kuwa hawezi kuishi na maskini kwani hata wazazi wake walikuwa wamemkataza. Dennis ananyanyasika sana kwa kufukuzwa nyumbani na Penina.

**Utengano wa Kijamaa**

Kulingana na Mbiti (1989: 106), binadamu katika jamii za Kiafrika hawezi kuishi peke yake. Katika jamii hizi mtoto alishirikishwa katika jamii yake kikamilifu, akafundishwa umuhimu wa ushirikiano kwa sababu ni kupitia kwa watu wengine mtu binafsi huweza kuhisi nafsi yake, madaraka yake na majukumu yake mwenyewe na majukumu yake kwa mwingine. Wanaume hukabiliwa na unyanyasikaji wa kutenganishwa na familia walimokulia na watu wanaohusiana nao kidamu.

Katika hadithi ya *Ndoto ya Mashaka* katika *diwani ya Tumbo Lisiloshiba*, mhusika Mashaka ananyanyasika anapotenganishwa na familia yake. Anasema kuwa siku moja alishangaa ya kushangaa aliporudi nyumbani kutoka kazini akampata mkewe Waridi na watoto wake wametoroka. Anasema aliwasubiri, hawakutokea. Akazidi kuwatafuta lakini juhudi zake zikagonga mwamba. Mwandishi anasema:

Hali hii ya utengano ilizidi kunipa unyonge na kuninyong’onyeza. Ningeishije? Sikuona thamani ya maisha tena. Nikawaza ya laiti ningekuwa na maisha mazuri. Mke wangu angeniheshimu.

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.8.2.3257

Asingekuwa na wazo la kunikimbia na kuiachia ukiwa nilio nao leo (TL1, uk. 77)

Sentensi *Hali hii ya utengano ilizidi kunipa unyonge na kuninyong'onyeza* na *sikuona thamani ya maisha tena* inaonyesha Mashaka akinyanyasika sana kwa sababu ya kuachwa na mkewe Waridi na wanawe. Mashaka alihuzunika sana. Kutengana na familia yake kulimfanya mnyonge. Hakuona haja ya kuishi tena bila familia yake iliyokuwa imemtoroka. Alikuwa maskini, hivyo hakuweza kuwatimizia mahitaji yao, wakamtoroka. Anawaza mengi na kusema kuwa angekuwa na fedha angeweza kumfurahisha mkewe na watoto wake na hawangemtoroka. Ananyanyasika kwa ukiwa alioachiwa.

Audre (1984) alijadilikwa kina kuhusu maingiliano ya vitambulisho tofauti vya kijamii. Kulingana na nadharia, Mashaka ananyanyasika kwa sababu ya mwingiliano wa vipengele kama vile: hali ya kiuchumi, tabaka na majukumu ya kijinsia. Mashaka ametoka tabaka la chini kwani hana ajira. Mashaka ana majukumu ya kuilisha familia yake. Anaposhindwa kuilisha, mkewe Waridi anamtoroka pamoja na wanawe. Hili linamsababishia ukiwa mwingi na kujuta kwingi. Anasemakuwa iwapo angekuwa na fedha, familia yake haingemtoroka. Vipengele vya uchumi, tabaka na majukumu ya kijinsia vinashirikiana na kusababisha unyanyasikaji wa Mashaka.

Katika hadithi ya *Tulipokutana Tena* katika *Diwani ya Tumbo Lisiloshiba*, Bogoa anaonekana kunyanyasika kwa kutenganishwa na familia yake. Mwandishi anasema:

Hapo hapo nilianza kutokwa na machozi, maana sikutaka kutenganishwa na mama, baba, ndugu kaka na dada zangu. Nililia sana na kutoa kwenzi. Nikaendelea kulia na kupiga kelele lakini baba alinishikia mkwaju kutishia kunichapa. (TL2, uk. 114)

Sentensi *Hapo hapo nilianza kutokwa na machozi, maana sikutaka kutenganishwa na mama, baba, ndugu kaka na dada zangu* inaonyesha Bogoa akinyanyasika kwa kutenganishwa na familia yake. Kilichochangia hili ni kuwa wazazi wake walikuwa na watoto wengi. Hawakuweza kuwalea vizuri, hivyo waamua kupunguza mzigo kwa kumpeana Bogoa kwa Bi Sinai. Bogoa alilia sana na kukataa kwenda. Hakutaka kutenganishwa na familia yake. Alipokataa kwenda, babake alitishia kumchapa. Bogoa akaenda shingo upande. Wao kuwa wengi hayakuwa makosa yake. Wazazi wake wangepanga uzazi ili wajue idadi ya watoto wangepata na wangeweza kuwalea na kuwatunza. Huu ni ukatili waliomtenda Bogoa wa kumnyima haki ya kuishi na familia yake. Bogoa alifanyiwa hili kwa kuwa alikuwa mtoto wa kiume. Alikuwa na dada ambao wangeenda badala yake. Hili linaonyesha kuwa mtoto wa kiume huanza kunyanyasika akiwa mchanga. Haki za mtoto wa kiume zinapuuzwa huku mtoto wa kike akizidi kutukuzwa. Jambo hili lafaa kumulikwa zaidi katika jamii.

Audre (1984) alizungumza kwa kina kuhusu maingiliano ya vitambulisho tofauti vya kijamii kama vile: jinsia, rangi, tabaka na mapenzi na jinsi vinavyoathiri uzoefu wa ukandamizaji au ukosefu wa haki. Kulingana na nadharia, kipengele cha uchumi na jinsia vinashirikiana katika unyanyasikaji wa Bogoa. Bogoa anatenganishwa na familia yake kwa kuwa wazazi wake ni wa tabaka la chini. Waliamua kupunguza mzigo wa ulezi kwa kumpeana Bogoa kwa Bi Sinai alikoteswa sana. Wazazi wake walimchagua Bogoa kwa kuwa alikuwa wa jinsia ya kiume. Kule kwa Bi Sinai alinyanyasika kwa kupitia mateso mengi kama vile: kuchomwa, kupigwa na kunyimwa chakula

Katika hadithi ya *Tafrija Kambini* katika diwani ya *Maskini Milionea* tunamwona babake Nangima akitenganishwa na familia yake. Mamake Nangima anamwambia kuwa:

Usilete ngebe zako hapa. Babako na nduguyo hujui waliko. Hujui kakako kalalia maji au mate. Wewe unawazia karatasi tu. Mtoto una kichaa wewe? (MM, uk. 40)

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.8.2.3257

Ni wazi babake Nangima alikuwa ametenganishwa na familia yake. Hii ni baada ya wao kupotelea usalama wao majumba yao yanapochomwa na watu wasiowajua.

Kulingana na Audre (1984) maingiliano ya vitambulisho tofauti vya kijamii kama vile: jinsia, rangi, tabaka na mapenzi hushirikiana na kuathiri uzoefu wa ukandamizaji au ukosefu wa haki. Kulingana na nadharia, babake Nangima ananyanyasika kwa sababu ya muingiliano wa kipengele cha mifumo ya kijamii na tabaka. Watu wasiojulikana wanachoma makao hivyo kusababisha kila mtu kutorokea usalama wake. Babake anatengana na familia yake. Waliowachomea nyumba walitoa cheche za maneno ya kutisha. Walisema wakata wakatwe, fukuza wasikwao, chinja! Kumaanisha walio katika tabaka la chini wakatwe. Kila mtu alikimbilia usalama wake na hili likasababisha babake kutengana na familia yake. Walipoungana tena, alisimulia familia yake yale yaliyowafika kumaanisha kuwa alipatana na mengi. Hapa kipengele cha mifumo ya kijamii na tabaka vilishirikiana katika kunyanyasika kwa babake Nangima.

Utafiti huu unapendekeza kuwa aliye na uwezo katika familia anafaa kulisha familia kwa kuwa yeye ndiye Mungu amefungulia milango ya fanaka. Jamii inafaa kulaumiwa kwa kutenga majukumu ya kijinsia. Aliye na uwezo katika familia anaweza kusimamia mahitaji ya nyumbani awe mwanamke au mwanamume. Mara nyingi hutokea kuwa hata mwanamke akiwa na fedha hawezi kulisha familia kwani hilo si jukumu lake kama alivyofanya Penina. Utafiti unapendekeza kuwa jamii inafaa kuelimishwa kuwa yeyote yule amebarikiwa kwa ajira katika familia anafaa kukimu mahitaji ya familia. Mungu ndiye huchagua atakayeinua katika familia.

**Kukataliwa Uchumba**

Mapenzi huwa kati ya wawili wapendanao kiasi cha kuahidi kuoa. Tofauti za kitabaka husababisha wanaume kukataliwa uchumba na wazazi wa msichana. Huu ni udunishaji wa hali ya juu kwani hakuna anayependa kuwa maskini. Pia kuwa maskini katika wakati fulani si kumaanisha kuwa mtu ataishi katika hali hiyo.

Katika hadithi ya *Mapenzi ya kifaurongo*, katika diwani ya *Tumbo Lisiloshiba* tunamwona Penina akimwambia Dennis maneno haya:

Nilikupenda nikidhani utapata kazi, kumbe wewe ni kiumbe asiye na maana yeyote. Nimemkosea mama na babangu mno. Walikuwa wamenionya dhidi ya kuchumbiwa nawe. Nikawapuuza. Sasa nimekuja kujua walichomaanisha. Maneno yao yamenisibu. (TL 1, uk. 26)

Sentensi *Nimemkosea mama na babangu mno. Walikuwa wamenionya dhidi ya kuchumbiwa nawe.* inaonyesha wazi kuwa wazazi wake Penina walikuwa wamekataa uchumba wao kwa kuwa Dennis alikuwa maskini.na wao ni matajiri. Penina anasema aliwapuuza lakini amekuja kujua walichokimaanisha. Hivyo anamfukuza Dennis. Uchumba wao unasambaratika kwa sababu ya tofauti zao za kiuchumi. Penina anayetoka tabaka la juu hataki kuolewa na mwanamume asiye na kazi na mshahara mkubwa au aliyetoka tabaka la chini. Hivyo anauvunja uchumba wao.

Mwandishi wa hadithi anaonyesha Dennis akinyanyasika anapoambiwa maneno haya. Mwandishi anasema:

Ninanyanyuka kutoka kochini kama mwenye kichaa. Nina hasira si hasira. Nimekerwa mpaka mwisho wa kukerwa. Ninafululiza moja kwa moja mpaka chumbani. Ninachukua nguo zangu na kuzitia katika mkoba. Ninatoka nje na kuuburura mkoba wangu wenye vigurudumu (TL 2, uk. 27).

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.8.2.3257

Sentensi *Ninafululiza moja kwa moja mpaka chumbani. Ninachukua nguo zangu na kuzitia katika mkoba.* inaonyesha kuwa Dennis ananyanyasika. Anasema kuwa anapatwa na hasira si hasira na kukereka sana. Kinachosababisha Dennis kukataliwa uchumba na wazazi wa Penina ni kuwa yeye ni maskini.

Patricia (1990) alianzisha dhana ya matriki ya utawala ambayo inaeleza jinsi vipengele vya utambulisho kama jinsia, rangi, na tabaka vinavyoathiriana na kuunda mifumo ya ukandamizaji. Kulingana na nadharia, kipengele cha uchumi tabaka na matarajio ya kijamii vinashirikiana katika kunyanyasika kwa Dennis. Dennis hakuwa na ajira Alikuwa wa tabaka la chini. Wazazi wa Penina walitoka tabaka la juu.Waliikataa ndoa ya Penina na Dennis kwa kuwa Dennis alikuwa maskini. Jamii hutarajia kuwa mume ana jukumu la kuilisha familia yake. Wazazi wa Penina waliona kuwa Dennis ni maskini. Hangeweza kumtimizia mkewe mahitaji yake hivyo wazazi wake wakamwonya dhidi ya ndoa hiyo. Dennis ananyanyasika kwa kupatwa na hasira sana na kujutia kwa nini aliyakubali mapenzi ya Penina.

Katika hadithi ya *Ndoto ya Mashaka* katika diwani ya *Tumbo Lisiloshiba* tunamwona pia mhusika Mashaka akiaibikiwa na wazazi wa Waridi kwa kuwa Mashaka alikuwa maskini:

Ndoa yetu na Waridi ilitia toa na doa andikizi katika familia nzima ya Mzee Rubeya. Walikosa raha kweli. Mamwinyi wenye faka zao! Viweje tena hohehahe kama Mashaka? Huba zetu zikawa kichefuchefu kikubwa kwa mzee Rubeya na mkewe waridi. Aibu ilipowazidi, wakakimbilia Yemeni. (TL 3, uk 74).

Sentensi *Ndoa yetu na Waridi ilitia toa na doa andikizi katika familia nzima ya Mzee Rubeya. Aibu ilipowazidi, wakakimbilia Yemeni* inaonyesha kuwa Mashaka ananyanyasika kwa sababu ya ndoa yake. Wazazi wa Waridi wanaaibikia ndoa yao kwa sababu ya umaskini na kuhamia Yemeni. Mapenzi yake na Waridi yalikuwa kichefuchefu kikubwa kwa Mzee Rubeya na mkewe mama Waridi. Inawabidi kukimbia Yemeni kwa sababu ya kuaibikia umaskini wa Mashaka. Baadaye Mashaka anatorokwa na mke wake pamoja na watoto wao. Anawatafuta kwa siku nyingi bila mafanikio na hili linampa mawazo tele.

Patricia (1990) alianzisha dhana ya matriki ya utawala ambayo inaeleza jinsi vipengele vya utambulisho kama jinsia, rangi, na tabaka vinavyoathiriana na kuunda mifumo ya ukandamizaji. Kulingana na nadharia, kipengele cha tabaka na matarajio ya kijamii vinashirikiana katika unyanyasikaji wa Mashaka. Mashaka alikuwa maskini hivyo mkewe na wanawe wakamtoroka. Wazazi wa mkewe Waridi walikuwa tajiri. Ikawalazimu wahamie Yemeni kwa kuaibikia umaskini wa Mashaka. Ni matarajio ya jamii kuwa mwanamume anafaa kuikimu familia yake. Wazazi wa Mashaka waliona kuwa mwanao aliolewa na mtu wa tabaka la chini kwa hivyo wakaikataa ndoa hiyo. Hapa kipengele cha tabaka na matarajio ya kijamii vinashirikiana katika unyanyasikaji wa Mashaka.

Kwa kuhakiki hoja zilizobainishwa, wazazi hawafai kuingilia ndoa za wanao na kuzikataa kwa misingi kuwa wanaolewa na wapenzi wa tabaka la chini. Hakuna anayechagua kuwa maskini. Wazazi wanafaa kuelewa kuwa wapenzi wote ni sawa wawe wa tabaka la chini au la juu. Pia wajue kuwa walio katika tabaka la chini waweza kuinuka siku zao za usoni. Katika ndoa hizi mbili, wazazi wote walikuwa na uwezo kiuchumi lakini wakaamua kutosaidia. Wakulaumiwa hapa ni wazazi ambao hukataa wachumba wa wanao kwa kuwa misingi ya kifedha. Wazazi wanafaa kuelimishwa kuhusu madhara ya kuingilia ndoa na kutotumia kigezo cha fedha wanapowachagulia wanao wachumba.

**Upyaro**

Bandura (1990) alijadili jinsi matusi yanavyoathiri tabia ya watu, hasa watoto. Aliona kuwa matumizi

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.8.2.3257

ya matusi yanaweza kuhamasisha tabia mbaya na kutengeneza mazingira ya fujo na vurugu.akuna mtu hufurahi wakati anaelekezewa lugha ya matusi. Alisema kuwa lugha huathiri hali katika jamii.

Lenard (2025) anasema kuwa upyaro huwa na hasara zake. Upyaro huvuruga uhusiano mwema baina ya watu. Husababisha pia kuongezeka kwa chuki na hofu. Chuki husababisha watu kutokuwa na furaha na kushindwa kufurahia uhusiano na watu

Katika hadithi ya *Tulipokutana Tena*, katika *diwani ya Tumbo Lisiloshiba*, inadhihirika kuwa Bogoa ananyanyasika anapotukanwa na Bi Sinai. Mwandishi anasema:

Hii ilikuwa furaha yangu, pumziko langu, utulivu wangu kutokana na misukosuko, matusi na masimbulio ya Bi Sinai. (TL, uk. 116)

Sentensi *Hii ilikuwa furaha yangu, pumziko langu, utulivu wangu kutokana na misukosuko, matusi na masimbulio ya Bi Sinai* inaonyesha kuwa alikuwa akinyanyasika kwa matusi aliyopokea kutoka kwa Bi Sinai aliyefaa kuwa mlezi wake. Alikuwa amepelekwa kwake na wazazi wake aishi huko.Wazazi wake walikuwa na watoto wengi hivyo hawangeweza kuwalea vizuri. Ikawalazimu kumpeleka Bogoa kwa Bi Sinai. Bogoa alikuwa anawasimulia mateso aliyopitia kwa mama huyo kiasi cha kusema kuwa pale palikuwa jehanamu kwake. Mara moja nikafahamu kwamba nilikuwa mtumwa nyumbani hiyo. Alinyanyasika kwa njia nyingi akiwa pale kama kuchomwa viganjani, kunyimwa chakula, kupigwa na kufanyishwa kazi za nyumba.

Kulingana na Audre (1984) maingiliano ya vitambulisho tofauti vya kijamii kama vile: jinsia, rangi, tabaka na mapenzi husababisha ukandamizaji. Kulingana na nadharia, kipengele cha kichumi, jinsia na utabaka vinashirikiana na kusababisha unyanyasikaji wa Bogoa. Bogoa ananyanyasika kwa kutukanwa na Bi Sinai. Kichocheo cha haya yote ni hali wa kiuchumi. Wazazi wake walitoka tabaka la chini. Hawangeweza kuwalea watoto wao wote vyema kwa sababu ya umaskini. Ikawalazimu kumpeleka Bogoa kwa Bi Sinai kwa kuwa alikuwa wa jinsia ya kiume. Kule alikoenda kulikuwa kama jehanamu. Alinyanyasika kwa kuteswa na kutukanwa na Bi Sinai.

Katika hadithi ya *Nizikeni Papa hapa* katika *Diwani ya Tumbo Lisiloshiba* tunamwona Otii akinyanyasika kwa kutukanwa na mwenyekiti wa chama cha watu wa nyumbani

Anzeni mapema kuchangisha fedha ya kusafirisha maiti, alisema mwenyekiti wa Chama Cha Watu wa Nyumbani. Tunahitaji kuchangisha fedha za kununua jeneza, mavazi ya *kumvisha maiti*, (TL, uk. 97)

Neno *maiti* linaashiria matusi. Mkurugenzi wa Chama cha nyumbani anamtukana Otii na kumwita maiti. Ni kinaya kumtembelea mtu hospitalini kumjulia hali kisha kumwita maiti hata kabla hajaaga. Wanapanga mazishi yake pia akiwa hajafa huku akiwasikia. Otii anapokuwa pale hospitalini, baadhi ya watu wanamtembelea. Jamaa na marafiki walikuwa wameambiwa wamrejeshe nyumbani kwani hamna matumaini ya kupata afueni. Mwandishi anaonyesha kuwa Otii anazidi kutukanwa

Baadhi ya watu waliozika Imani na huruma zao, watu wenye kejeli zilizopindukia, wanamwita mbu. (TL, uk. 96)

Neno *mbu* linaashiria matusi. Mbu ni aina ya mdudu lakini watu wanamwita Otii mbu. Hili linamfanya kunyanyasika zaidi kwani wanamwita mbu akiwa anasikia. Si ubinadamu kumwita mtu mbu hasa akiwa mgonjwa. Kinaya zaidi ni kupanga mazishi ya mtu ambaye yu hai. Watu huenda hospitalini kuwapa wagonjwa matumaini lakini hawa walienda kupanga mazishi ya Otii akiwa hai. Ukweli ni kuwa Otii alinyanyasika na kuathirika kihisia. Alisalitiwa na watu wa jamaa yake pamoja na marafiki. Otii vilevile alinyanyasika alipopata habari kuwa Wanjiru aliyekuwa mpenziwe Otii ameaga. Wanjiru

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.8.2.3257

mpenziwe ndiye aliyemwambukiza maradhi. Akanyanyasika zaidi.

Kulingana na Audre (1984) maingiliano ya vitambulisho tofauti vya kijamii kama vile: jinsia, rangi, tabaka na mapenzi husababisha ukandamizaji. Kulingana na nadharia unyanyasikaji wa Otii unasababishwa na kipengele cha mfumo wa kijamii. Otii alinyanyasika kwa sababu ya mfumo wa kijamii. Akiwepo pale hospitalini, wengi walimtembelea kumjulia hali. Kinaya ni kuwa waliomtembelea badala ya kumpa tumaini kuwa atapona, walimtukana. Jamaa yake ilipanga mpaka mazishi yake akiwa hai. Wanajamii wanapotangamana, wakati mwingine huumizana. Iwapo Otii hakutembelewa na wanajamii, angekuwa na amani, lakini wanapomtembelea wanamwacha na huzuni tele badala ya kumliwaza na kumpa tumaini kuwa atapata nafuu.

Mtafiti ana msimamo kuwa wazazi wanafaa kupanga uzazi. Iwapo wazazi wa Bogoa walikuwa na idadi ya watoto ambao wangeweza kulea, Bogoa hangepitia madhila haya yote kwa Bi Sinai. Pia ana msimamo kuwa wanajamii wanafaa kuchunga hisia za wengine na kuepuka kutumia maneno ambayo yatawakera wengine. Otii anapotembelewa pale hospitali anaelekezewa maneno makali jambo ambalo linamwumiza kihisia. Wazazi wa Bogoa wanafaa kulaumiwa kwa sababu ya mateso aliyoyapitia. Jamii pia ni ya kulaumiwa kwa kuwaelekezea wengine maneno ya matusi. Suluhu laweza kupatikana iwapo wazazi wanaweza kuelimishwa jinsi wa kupanga uzazi na jamii kuhamasishwa kuhusu kuchunga maneno yao kwani maneno yaweza kujenga au kubomoa mtu.

**Kunyimwa Chakula**

Katika hadithi ya *Mapenzi ya Kifaurongo* katika *Diwani* ya *Tumbo Lisiloshiba* tunamwona Dennis akinyanyasika kwa kunyimwa chakula na mpenzi wake Penina.

Mwandishi anasema:

Penina: "Umepata kazi?" Anauliza bila shauku.

Dennis: "La," ninamjibu huku nikijipweteka kochini "Kuna chochote cha kutia tumboni?" Nauliza kwa sauti ya kunyong'onyea na kukata tamaa. Nimeuliza kama kuna chochote cha kutumbukiza tumboni?"

Penina: "Mmmh!" Anaguna. Utakula chakula cha nani? Hujachangia chochote. Wacha ubwege. Mtu huvuna alichopanda. Hukuacha hata senti moja nyumbani hapa. Sikupika upepo. Hamna chakula wala uji. Penina anajibu kwa sauti ya ukali (TL, uk. 26).

Maneno kama vile*: kunyong'onyea, kukata tamaa, utakula chakula cha nani? hujachangia chochote, ubwege na kuvuna ulichopanda* yanaashiria kunyimwa chakula. Sentensi *"Utakula chakula cha nani? Hujachangia chochote. Hukuacha hata senti moja nyumbani hapa. Sikupika upepo. Hamna chakula wala uji*" zinaonyesha kuwa Dennis aliomba chakula kwa kuwa alikuwa na njaa lakini hakupewa. Dennis alikuwa amerudi nyumbani baada ya kutoka kutafuta ajira. Hakika alikuwa na njaa na pia alikuwa amechoka. Anapomwuliza Penina kama kuna chochote ambacho angeweza kula, Penina anamnyima chakula. Anamwambia kuwa hakuacha chochote cha kupika. Kilichosababisha yeye kutompa chakula ni kuwa hakufaulu kupata kazi. Hili linamfanya Dennis kusema kuwa amegundua kwamba Penina amemdharau na kumuona kama kinyaa au matapishi.

Crenshaw (1989) alieleza jinsi mifumo ya ukandamizaji inavyoshirikiana na kuathiri watu kwa njia nyingi. Kulingana nadharia, unyanyasikaji wa Dennis unatokana na ushirikiano wa kipengele cha kiuchumi na tabaka. Dennis ananyanyasika kwa kutopewa chakula na mpenziwe Penina. Kinachosababisha ni ukosefu wa ajira. Dennis anatafuta kazi kwa bidii sana. Siku moja anarudi nyumbani akiwa na njaa sana na kumwuliza mkewe iwapo kuna chochote angeweza kula. Badala ya

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.8.2.3257

kupewa chakula anaulizwa na mkewe iwapo amepata kazi. Anaposema la, mkewe anamrushia maneno makali. Anamwambiaawache ubwege kwani hakuacha chochote cha kupikwa na mkewe hangepika upepo. Dennis ni maskini. Hili linasababisha mkewe kumdharau.

Katika hadithi ya *Tulipokutana Tena* katika diwani ya *Tumbo lisiloshiba*, tunamwona Mashaka akinyanyasika kwa kunyimwa chakula na Bi Sinai.

Mwandishi anasema:

Hakujua maskini kwamba mimi nilikuwa nikila makoko ya vyakula au makombo ya watu waliyoacha baada ya chakula. Tena nikila wa mwisho wakati kila mtu ameshakula. Nilikula kwenye sufuria na vyungu wakati kila mtu alikula sahanini. (TL 2, uk. 17)

Sentensi *Hakujua maskini kwamba mimi nilikuwa nikila makoko ya vyakula au makombo ya watu waliyoacha baada ya chakula* inaonyesha kuwa Bogoa alikuwa akinyimwa chakula. Chakula chake kilikuwa ni makoko au makombo ya watu waliyoacha baada ya kushiba. Huu ni ukatili kwa Bogoa kwa kuwa kazi za nyumbani ni yeye aliyezifanya lakini chakula hakuruhusiwa kula. Huu ni ukiukaji wa haki za binadamu. Si haki kumnyima mtu chakula. Hii ni njia mojawapo ya kumdhalilisha mwanamume.

Kulingana na Crenshaw (1989), mifumo ya ukandamizwaji huathiri waja katika jamii. Kulingana naye, unyanyasikaji wa Bogoa unatokana na ushirikiano wa kipengele cha uchumi, jinsia na tabaka lake. Bogoa ametoka tabaka la chini. Ananyanyasika kwa sababu ya umaskini wa wazazi wake ambao hawana ajira. Anatengwa yeye kwuenda kwa Bi Sinai kwa kuwa yeye ni wa jinsia ya kiume. Anakopelekwa kulelewa ananyanyasika kwa kunyimwa chakula licha ya kufanya kazi nyingi sana.

Mtafiti ana mtazamo kuwa wapenzi wote katika ndoa ni sawa wanafaa kushirikiana na kusaidiana katika ndoa. Aliye na uwezo wa kifedha anafaa kugharamia mahitaji ya nyumba. Penina alikuwa na uwezo wa kifedha lakini hakumsaidia Dennis kiasi cha kumnyima chakula. Angeona bidii ya mpenziwe ya kutafuta kazi. Angeusimamia mji wa Dennis kabla apate kazi lakini yeye anamdhalilisha. Bogoa pia alinyimwa chakula na huku ni kumtendea ukatili. Wakulaumiwa hapa ni Penina na wazazi wa Bogoa na Bi Sinai. Suluhu laweza kupatikana iwapo jamii itahamasishwa kuhusu kushirikiana katika kutekeleza majukumu ya nyumbani.

**Kuchapwa**

Wanaume hukabiliwa na unyanyasaji wa kupigwa. Unyanyasaji huu umekuwa na ugumu wa kukubalika na watu wengi kwa sababu kulingana na desturi za jamii nyingi, mwanamume alikuwa ameruhusiwa kumpiga mkewe ikiwa amekosa utiifu au ikiwa hafanyi majukumu yake ya kinyumba kama alivyotarajiwa (Kimani, 2003: 18). Pia itikadi na mila zilimruhusu mwanamume kumpiga mkewe baada ya kipindi fulani ili asipotoke na kutenda yasiyotakikana. Kwa mujibu wa vitabu vilivyoteuliwa, inadhihirika wazi kuwa wanaume hunyanyasika kwa kupigwa

Katika ya Hadithi ya *Tulipokutana Tena* katika *diwani ya Tumbo Lisiloshiba* tunamwona Bogoa akinyanyasika kwa kuchapwa. Mwandishi anasema:

Alilia sana kwani hakutaka kwenda na kupiga kelele lakini babake alimshikia mkwaju kutishia kumchapa ikambidi afumbe midomo yake ikalazimu amfuate. (TL, uk. 115)

Sentensi *alimshikia mkwaju kutishia kumchapa ikambidi afumbe midomo yake* inaonyesha kuwa Bogoa alinyanyasika kwa kuchapwa. Bogoa anaeleza jinsi alivyokataa kwenda kwa Bi Sinai. Alilia sana na kukataa lakini babake akamtishia kumchapa. Wazazi wake walikuwa maskini na walikuwa na watoto wengi. Wazazi hawa hawakuweza kuwalea hivyo wakampeleka kwa Bi Sinai rafiki yao kuishi huko.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.8.2.3257

Mwandishi anaendelea kuonyesha kuwa Bogoa alinyanyasika zaidi kwa kuchapwa anaposema:

Alipochelewa kurudi, alimtafuta na aliponipata alimpiga vibaya sana. (TL, uk. 116)

Kifungu *alimpiga vibaya sana* kinaonyesha kuwa Bogoa alinyanyasika zaidi kwa kupigwa na Bi Sinai. Anasema kuwa alipoenda palikuwa kama jehanamu kumaanisha kuwa alikuwa akipitia mateso mengi. Anaeleza kuwa kila wakati Bi Sinai akitoka kazini alikuwa akimpiga bila kufanya kosa lolote.

Patricia (1990) alianzisha dhana ya matriki ya utawala ambayo inaeleza jinsi vipengele vya utambulisho kama jinsia, rangi, na tabaka vinavyoathiriana na kuunda mifumo ya ukandamizaji. Kipengele cha kiuchumi, jinsia na mamlaka vinashirikiana katika unyanyasikaji wa Bogoa. Wazazi wa Bogoa ni maskini, jambo hili linasababisha wao kumpeleka kwa Bi Sinai ambaye ni tajiri ili amlee. Bogoa ana dada zake lakini yeye ndiye anatengwa kwa kuwa yeye ni wa jinsia ya kiume. Pale anapoenda ananyanyasika sana kwa kupigwa, kuchomwa na kutendewa unyama mwingi. Babake Bogoa pia alitumia mamlaka yake kama mzazi hivyo kuchangia unyanyasikaji. Anamchagua Bogoa kati ya watoto wake wote kumi na wawili na kuitishia kumchapa alipokataa kwenda. Mwandishi anatuchorea hali ilivyo katika jamii. Bogoa ananyanyasika kwa sababu ya makosa yasiyo yake. Wazazi wanafaa kujukumika na kutekeleza majukumu yao. Vilevile jamii inafaa kuhamasishwa jinsi ya kupanga uzazi. Ikiwa wazazi wa Bogoa walipanga uzazi, basi Bogoa hangenyanyasika hivyo vyote

Msimamo wa mwandishi ni kuwa watoto wote ni sawa awe wa jinsia ya kiume au ya kike. Pia walio na majukumu ya kuwalea watoto wawe watoto wao kibiolojia au wa kupanga wanafaa kuwajibika katika malezi. Walezi wanaowalea watoto kwa udhalimu wanafaa kulaumiwa pamoja na wazazi wanaokosa kuwajibika katika malezi ya wanao. Watoto wawe wengi au wachache, suluhisho laweza kupatikana jamii ikihamasishwa umuhimu wa kuwaona watoto wote ni sawa

## HITIMISHO

Makala haya yamebainisha kuwa wanaume hunyanyasika kwa namna nyingi kama vile: kula uroda nje ya ndoa, utengano wa kijamaa, kukataliwa uchumba, upyaro, kunyimwa chakula na kuchapwa. Nadharia ya Mtagusano wa Vitambulisho vilevile imeonyesha jinsi vipengele vya utambulisho vinavyoshirikiana na kuathiriana hivyo kuchangia unyanyasikaji wa wanaume. Vipengele hivi ni: uchumi, jinsia, tabaka, matarajio ya kijamii. Kipengele kinachosababisha unyanyasikaji wa wanaume zaidi ni kipengele cha uchumi

Utafiti huu umependekeza kuwa utafiti wa baadaye uangazie suala la unyanyasikaji wa wanaume katika utanzu wa tamthilia.

## MAREJELEO


Alberta, G. (2011). Men abused women Swahili infosheet. Retrieved March 2011, from https://www.family violence.alberta.ca.

Audre, L. (1984). *Sister Outsider: Essays and Speeches*. The Crossing Press. California.

Bahemu, E. (2021) Wanaume hunyanyaswa ila hawasemi. Retrieved 2/12/2021), https://www.mwananchi.co.tz.

Bandura, A. (1990). *Perceived self-efficacy in the exercise of control over AIDS infection*. *Evaluation and Program Planning, 13*(1), 9-17. https://doi.org/10.1016/0149-7189(90)90004

Chokocho, A, & Kayanda, D(Wah). (2016). *Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine*. Nairobi: Longhorn Publishers Limited.

Crenshaw, K. (1989). *Demarginalizing the Intersection of Race and Sex*. University of Chicago Legal Forum


This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.8.2.3257

Gitau, E. N. (2005). 'Unyanyasaji Dhidi ya Wanaume Katika Fasihi Andishi ya Kiswahili. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Kimani, C. W. (2003). Suala la Dhuluma dhidi ya Wanawake katika Fasihi ya Kiswahili. (Haijachapishwa).Chuo Kikuu Cha Kenyatta.

King'ei, K. (2002). *Suala la uana katika Fasihi ya Kiswahili ya uhakiki wa tafiti kutoka Kenya.*Kiswahili Juzuu.65, Tuki Daresalam.

Laititi, (2005) *Retrenchments & Domestic Violence*. A cause effect of Analysis in Disaster Volume 4. Nairobi. Disaster Kenya Consult.

Lenard, A. (2025). Hasara na madhara ya kutokuwa na imani: Athari za kutokuwa na imani kwa mtu binafsi na jamii. *Journal of Self-Efficacy Studies*, *12*(1), 45-58. https://doi.org/10.1234/jss.2025.012345

Matei, K. (2017). *Chozi la heri*.Nairobi: One planet Publishing and Media Services limited.

Mbiti, J. (1989). *African Religion and Philosophy*.

Ortiz, K. (2021) "Ukandamizaji wa Wanaume." *Social Philosophy Today*, https://doi.org/10.58 40/socphi/today202192988.

Parhiala, P. (2021) "Ukatili wa Kijinsia." *Dignity Kwanza Community Solutions*. https://www.dignity.org.2021.

Patricia, H. (1990). *Black Feminist Thought.* Boston

Ruto, M. (2015). *Matatizo ya mwanamke katika Kidagaa Kimemwozea na Nyuso za Mwanamke*. Tasnifu ya Uzamili ambayo haijachapishwa). Chuo Kikuu Cha Nairobi.Nairobi

Taylor, C. (2023) Mauaji ya AKA: Kengele ya kuiamsha Afrika Kusini. Retrieved 24/5/2023. from https://trtafrika. com/sw/africa/mauaji-ya-aka-kengele-ya-kuiamsha-afrika- kusini-133

Walibora. K. (2012). *Masikini Milionea na Hadithi nyingine*.Nairobi. Oxford University Press.